Rasimu ya taarifa ya majibu huru ya watu ya Mkutano wa kilele wa mifumo ya vyakula ya Umoja wa mataifa (UN.)

Kutatua migogoro ya chakula duniani, tunahitaji mabadiliko halisi ya mifumo ya vyakula kwa ajili ya watu na dunia.

Mkutano wa kilele wa Mifumo ya vyakula ya Umoja wa Mataifa utaendeleza kwa haraka zaidi mifumo ya vyakula inayoendeshwa na ushirika wa viwanda.

Ujumbe muhimu:

- Kutatua migogoro ya njaa ya dunia na utapiamlo kunahitaji hatua za haraka na zilizoratibiwa ambazo zitakidhi mahitaji, haki na mahitaji ya walioathirika zaidi.
- Mkutano wa kilele wa Mifumo ya vyakula wa Umoja wa mataifa haukuzipuuza haki hizi na mahitaji tu, na sababu za kimuundo za migogoro lakini pia imefichua mfumo wa “biashara kama kawaida”, uimarishaji wa mifumo ya vyakula ya ushirika wa viwanda kama ni hatua zenye kuleta mabadiliko.
- Mkutano wa kilele wa mifumo ya vyakula wa kuhesabu hisa ya vyakula wa umoja wa mataifa (UNFSS) umelenga kuaangalia mapungufu ya mkutano wenyewe, pia kufungua milango ya Umoja wa mataifa kwa kampuni zenye ushawishi mkubwa zaidi na mitandao yao, bila ya kuwa na mfumo wa uwajibikaji wa shirika/kampuni.
- Utata mkubwa uliopo kwa UNFSS upo baina ya/unatokana na mifumo ya vyakula inayoendeshwa na viwanda yenye kudumu na misingi ya lazima ya haki za binadamu, mifumo ya mabadiliko ya vyakula ya kiagroekolojia (kilimo hai) kuelekea uhuru wa vyakula.
- Kuikabili UNFSS, harakati za kijamii, wenyeji (wazawa) na asasi za kiraia duniani kote wanaeleza tena wasiwasi wao mkubwa kuhusu kuimarishwa kwa nguvu ya shirika/kampuni ndani ya Umoja wa mataifa UN, kuongeza mahitaji yao kwa mabadiliko halisi ya mifumo ya vyakula na wito kwa kuimarishwa kwa mfumo wa kimataifa wa kidemokrasia.

Mkutano wa kilele wa mifumo ya vyakula wa umoja wa mataifa (UN) wa kuhesabu hisa ya vyakula.

Umepangwa kufanyika tarehe 24-26 Rome, Mkutano wa kilele wa mifumo ya vyakula wa kuhesabu hisa za vyakula wa UN ni tukio la katibu mkuu wa Umoja wa mataifa, mwenyeji wake ni Rome na limepangwa kwa kushirikiana kwa taasisi za UN nchini Rome. Mkusanyiko huu utahudhuriwa na watu mashuhuri mbalimbali wakiwemo kutoka katika taasisi za Umoja wa mataifa (UN), wakuu mbalimbali wa nchi, na wawakilishi wengine wa nchi wanachama.

Mkutano wa kilele wa mifumo ya vyakula wa kuhesabu hisa ya chakula wa UN (UNFSS) umelenga kuaangalia mapungufu ya mkutano wenyewe, pia kufungua milango ya UN kwa kampuni zenye ushawishi mkubwa zaidi na mitandao yao, bila ya kuwa na mfumo wa uwajibikaji wa shirika/kampuni.

Mkutano wa kilele wa mifumo ya vyakula wa kuhesabu hisa za vyakula **umejengwa kudharau** mahitaji ya kiundani zaidi ya mabadiliko ya kimuundo katika mifumo yetu ya vyakula, ikitilia mkazo zaidi badala yake mfumo ambao unaipa kipaumbele utengenezaji wa faida zaidi kuliko maslahi ya umma.

Kwa takriban miaka mitatu iliyopita, makundi mengi – harakati za kijamii, wenyeji, vijana, wanawake na watu wa jinsia tofauti, wametoa pendekezo thabiti na mahitaji kwa ajili ya muendelezo wa kilimo hai, uhuru wa chakula, viumbe hai, haki za jinsia na utofauti na shirika la vijana, haki ya hali ya hewa, haki ya kiuchumi na kijamii ndani ya mifumo ya vyakula.

Mapendekezo haya yamepuuzwa mfululizo, muundo ambao umeendelea mwaka 2021 na kuongezeka mwaka 2023. Jambo ambalo linahusiana hasa na kuongezeka kwa njaa na utapiamlo, kuongezeka kwa ukosefu wa usawa, na migogoro iliyopo ambayo binadamu na dunia inakumbana nayo. Dhidi ya hali hii, asasi za kiraia na shirika la wenyeji (wazawa) kwa mara nyengine tena wanapaza sauti zao kupitia taarifa hii ya umma.

Mtazamo muhimu wa nyuma juu ya mkutano wa kilele wa mifumo ya vyakula

Miaka miwili iliyopita, mkutano wa kilele wa mifumo ya vyakula ya Umoja wa mataifa ulikumbana na uhamasishaji wa kukabiliana ambao haujawahi kutokea wa washiriki zaidi ya 9,000 wakiupa changamoto mkutano wa kabla wa kilele, mwezi julai mwaka 2021. Makundi kutoka maeneo/mikoa yote walitoa ushuhuda juu ya hatua za awali wanazozichukua kubadili namna ya utoaji wa vyakula. Idadi kubwa ya watendaji kutoka asasi za kiraia,wazalishaji wadogo wadogo wa chakula, na wafanyakazi kutoka katika mashirika, wenyeji wa asili (wazawa), wanawake na vijana, serikali, wanataaluma na Umoja wa mataifa, pamoja na watu wenye uzoefu kutoka ndani na nje ya mkutano wa kilele walionesha kutoridhishwa na muundo wake, mwelekeo wa kisiasa na mchakato wa kuandaa ambao, kutokea mwanzo ulionesha kudhoofisha mafanikio ya demokrasia ya pande nyingi yaliyofanywa na walioifanyia marekebisho kamati ya Umoja wa mataifa ya Usalama wa chakula duniani.

Tamko la kisiasa lililopelekwa kwa mkutano wa kilele wa mifumo ya vyaakula duniani mwezi septemba 2021 lilidhoofishwa na zaidi ya mashirika ya kimataifa na kitaifa mia saba (700) , na zaidi ya wanataaluma na wanaharakati mia tatu (300). Ujumbe muhimu wa kupinga uhamasishaji uliungwa mkono kupitia mamia ya karatasi za kitaaluma, machapisho kwenye

mitandao ya kijamii na kutajwa kwenye vyombo vya habari duniani kama vile BBC, Al Jazeera, Italian State TV Rai, Le Monde, El Pais, The Guardian, Deutshe Welle, nakadhalika.

Ijapokua, “Mkutano wa kilele wa watu” (Kama waandaaji walivoita), na waliochanganyikiwa, mchakato wa msingi wa ushirika unaoongoza kwake, uliwakatisha tamaa watu uliyopasa kuwatumikia. **Mkutano wa kilele ulishindwa kutaja vichochezi muhimu** vya ukuaji wa njaa duniani na migogoro ya hali ya hewa, hasa janga kubwa la ugonjwa wa COVID-19, kilimo cha viwanda na mkusanyiko wa ushirika katika mifumo ya vyakula.

Kwa mtazamo wake wa wadau walio wengi, **mkutano wa kilele uliwakosea nchi wanachama na mataifa kwa ujumla**. Wakati maofisa wakuu wa Umoja wa mataifa, baadhi ya serikali hasa kutoka nchi za OECD, pamoja na mtandao wa mashirika, wahisani na wanataaluma wenye urafiki na ushirika na taasisi zisizo za kiserikali walitumia ushawishi mkubwa kwenye mchakato wa mkutano wa kilele na maudhui yake, namba kubwa ya nchi wanachama, hasa kutoka mataifa ya kusini walitengwa.

Kubwa zaidi, **mkutano wa kilele ulizikosea haki za binadamu**. Ukosoaji wa haki za binadamu dhaifu za ndani ya mkutano huo zilielezwa kwa ufasaha na mara nyingi na **watendaji** mbalimbali wa ndani na nje ya mkutano lakini zilipuuzwa mfululilizo. Sambamba na hayo, mkutano pia ulidhoofisha mafanikio yaliyopiganiwa sana ya kidemokrasia zaidi ya utawala wa vyakula wa dunia, kama kamati ya usalama ya Chakula ya Umoja wa mataifa (CFS) na shirikisho lake la sayansi na sera, pamoja na jopo kubwa la wataalamu (HLPE).

Miaka miwili baadae: Hakuna mabadiliko katika mwelekeo.

Kufuatia mkutano wa kilele wa mifumo ya vyakula ya Umoja wa Mataifa wa mwezi septemba 2021, hatua muhimu zilichukuliwa kuhakikisha ufuatiliaji wake, ijapokua **mpango wa utekelezaji wa mkutano huo ulikua ni tamko la katibu mkuu wa Umoja wa mataifa** ambao haukujadiliwa wala kuthibitishwa na mchakato wa baina ya serikali.

Licha ya ahadi za wazi za Naibu katibu mkuu wa umoja wa mataifa kabla ya mkutano **kwamba hakuna muundo mpya utakaoundwa, kitovu cha uratibu cha mifumo mipya ya vyakula ya Umoja wa mataifa ulianzishwa**, wenyeji wao walikua Rome na kwa pamoja ukaongozwa na Naibu katibu mkuu wa umoja wa mataifa na wakuu wa FAO, WFP, IFAD, WHO na UNEP. Na muundo mpya ukapatiwa bajeti ya miaka miwili ya dola za kimarekani milioni kumi na nne (14), ikiwa ni zaidi ya **mara mbili ya bajeti ya CFS**.

Kwa hakika, usanifu wa kitovu cha uratibu **hauhusishi serikali za kitaifa ndani ya muundo wake wa utawala**. Inahusisha shirikisho jipya la sayansi na sera, pamoja na uteuzi mpya wa

wadau na kundi la ushauri wa mitandao (SENA) ambalo limezidisha kazi kwa CFS na HLPE. Ijapokua, imeshindwa kuheshimu haki za asasi za kiraia kama shirika la kujitegemea na kupitisha ajenda ya upendeleo kuelekea kuimarisha mtazamo wa kirafiki wa viwanda wa mkutano wa kilele wa mifumo ya vyakula, ambapo majadiliano juu ya taratibu au mapungufu juu ya kupanuliwa kwa shirika/viwanda na mkusanyiko haukuwepo dhahiri.

Lengo kuu la tukio la FSS+2 ni kutaja/kueleza na kutatua **ukosefu/upungufu wa uhalali** wa mkutano wa awali wa kilele: kwa ukweli kwamba **haukufanywa kama mkutano baina ya serikali**, kama mkutano wa chakula wa Umoja wa mataifa wa mwaka 1996, 2002 na 2009, na hivyo haukuhitimishwa kwa tamko la makubaliano baina ya serikali na mpango kazi. Nchi wanachama waliombwa kueleza njia za kitaifa wanazotumia kubadili mifumo ya vyakula katika nchi zao, lakini baadhi ya nchi walihusishwa katika kufafanua matokeo ya mkutano wa kilele.

Kuna **wasiwasi ulionea kwamba mkutano wa mifumo ya vyakula utajidhihirisha kuwa wao ni "nunua katika mtego"** ambapo serikali itatoa msaada katika mchakato mzima wa mkutano wa mifumo ya vyakula kwa kushiriki kwa wingi na kwa shauku ya kutaka kuonesha mikakati yao ya kitaifa ya mifumo ya vyakula. Hili litatokea bila ya kujali ni kwa namna gani njia zao za kitaifa zimeendelezwa kupitia mashauriano mjumuisho, ni mwelekeo upi wanaelekea, au hatakama wametekeleza.

Mkutano wa mifumo ya vyakula hautazami matokeo ya makubaliano baina ya serikali na kusahau majibu ya pamoja ya migogoro ya vyakula ya dunia. Badala yake, tukio limelenga kuunda udanganyifu ulioenea wa msaada wa serikali, **unaopelekea uhalisia na uhalali wa zamani wa mchakato wa mkutano wa mifumo ya vyakula ya umoja wa mataifa**, hivyo kuhalalisha muundo wake wa mara mbili na kudumisha ajenda ya mifumo ya vyakula inayoendeshwa na kiwanda.

Uchambuzi wa hivi karibuni umeutathmini mkutano wa mifumo ya vyakula kwa muktadha mpana wa kuongezeka kwa ushawishi wa shirika juu ya utawala wa vyakula duniani, kama inavyoonekana kwa tukio ambalo halijawahi kutokea la shirika la chakula duniani la sera ya mlango wazi kwa sekta ya viwanda, jukwaa la chakula la dunia, mpango wa mkono kwa mkono na mbinu ya jumla ya wadau walio wengi na ushiriki unaodhibitiwa.

Mabadiliko ya mifumo ya vyakula halisi kwa ajili ya watu na dunia ni ya haraka na inawezekana

Mnamo mwaka 2022, takriban watu milioni mia mbili hamsini na nane (258) walikumbana na ukosefu wa chakula usio wa uhakika, kutoka watu milioni mia moja tisini na tatu (193) kwa mwaka 2021 na watu milioni mia moja hamsini na tano (155) kwa mwaka 2020. Migogoro hii ya kimfumo inayoendelea ni matokeo ya kushindwa kwa sera na kuachwa, na ni matokeo ya

kufuata njia yenye shaka ambayo huzidisha ukosefu wa usawa/ubaguzi na utegemezi, na kumiminika athari nyingi zinazozidisha madeni ya dunia na migogoro ya hali ya hewa.

Moyo wa mabishano upo kwenye **migongano** baina ya **uendelezaji wa shughuli za viwanda/ushirika** na umuhimu kwa **misingi ya haki za bindamu,mabadiliko ya mifumo ya vyakula ya kiagroikolojia kuelekea uhuru wa chakula/vyakula.**

Kwa nyakati hizi za migogoro mingi iliyoambatana, serikali pamoja na Umoja wa mataifa ichukue hatua za haraka zaidi kuliko hapo awali kwa kusikiliza sauti za majimbo yaliyoathirika zaidi, kubadilisha muelekeo, na kusaidia mahitaji yao na jitihada kwa mabadiliko ya mifumo ya vyakula kwa ajili ya watu na dunia, kwa kuzingatia heshima kwa haki zote za binadamu, na kuendeleza/kukuza kilimo hai, uhuru wa vyakula, viumbe hai, haki za jinsia na utofauti, shirika la vijana, haki za hali ya hewa, haki za kiuchumi na kijamii, katika vipimo/Nyanja vyote vya mifumo ya vyakula.